# LEARNING BY EAR

## ”MGENI KIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA”

**KIPINDI CHA SABA: ”NI WASAA WA KUPONA”**

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**HEALTH EXPERT: DR. HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 7:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- ZAWADI (BABY, no actor)
- DR. MUNGA (45)
- MIZANJA (65)
- MAMA DAVID (43)
- NURSE (24)
- HEADTEACHER (38)
- RADIO PRESENTER (28)

**INTRO/NARRATOR (same voice):**
Nawasalimu tena wasikilizaji na asanteni kwa kujiunga nasi katika kipindi hiki cha **noa Bongo jenga maisha yako,kwenye mchezo " WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA"**. Katika kipindi kilichopita, tuliiacha Familia ya Masika hospitalini ambako Karembo alikuwa amelazwa kwa homa kali ya malaria... wote wakahimizana kufanyiwa utafiti wa damu ilikujuwa ikiwa wanaugua malaria au la... usisahau pia walikuwa na mvutano na jirani yao mkubwa mamake david. Je, ni yupi aliye salama na vimelelea hivyo vya malaria?na je Karembo atapata afueni?, Kwa uhondo zaidi usibanduke katika kisa cha leo '' **NI WASAA WA KUPONA"** Ni usiku wakati Masika akiwa nyumbani kwake anasikiliza redio yake...

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: MASIKA AT HIS HOUSE LISTENING TO RADIO</u>**

**A-SFX:BUZZING OF MOSQUITOES THEN RADIO BEING TUNED**

1. **RADIO PRESENTER:**

Katika taarifa zetu nyengine zilizotufikia hapa studioni , tumearifiwa kuwa kuna mkurupuko wa ugonjwa wa malaria katika eneo la Ribo na vitongoji vyake unaoleta zahama kwenye hospitali ambazo tayari zimejaa pomoni wagonjwa wa malaria. Hii ni kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na itikadi duni za wavuvi za kutumia neti za kujikingia mbu kwa kuvulia samaki. Leo hapa studio tumetembelewa na Dkt.Munga ambaye atatupa usahauri zaidi baada

ya taarifa hii ya habari katika kipindi cha " Maisha bora".

2. **B-SFX:BUZZING OF MOSQUITOES AGAIN FOLLOWED BY SLAPS**

**NARRATOR:** Masika alilitega sikio lake huku akijutia kitendo chake cha kuichukuwa neti ya kukingia mbu kutoka kwa mke wake na mtoto na badala yake kuwahimiza pasi kujuwa wavuvi wengine. Akitafakari na kujiuliza ni vipi vipimo havikumuonyesha kuwa na malaria isipokuwa mkewe na Zawadi damu zao zilionyesha malaria kwa uchache na daktari Munga aliwapatia dawa ili kuwatibu. Atafanya nini kuzuia uhaini alioufanya? Je, wavuvi watamsikiza? Kabla ya kujijibu haya makala ya " maisha bora" yalikuwa yameanza....

3. (**RADIO TRANSMISSION CONTINUES..)**

4. **RADIO PRESENTER:**

Hamjambo jioni ya leo na karibuni katika kipindi cha Maisha bora. Tunaye studio Dkt. Munga anayezungumzia kuhusu janga la malaria katika eneo letu.sasa bwana dkt hebu waeleze wasikilizaji kama bingwa wa utabibu wa malaria, kweli unafikiria kuna mkurupuko wamalaria au ni porojo tu? Na kama ni kweli upo.. suluhisho ni nini?

5. **DR. MUNGA:** Shukran,

(**CLEARS THROAT)**

kwanza kabisa, mimi na wauguzi wenzangu tumechunguza na kupata kwamba wengi wa

wagonjwa wa malaria hawaji hospitali kwa wakati unaofaa.. wengi wao huja kipindi ambacho malaria imekuwa nyingi mno mwilini na hii ni hatari! Sasa katika kukujibu swali lako, mbu hutaga na kuzaana wengi msimu wa mvua na hususan sehemu zinazokaa maji, nyasi ndefu au kichaka na iwapo hakuna lolote litakalo fanywa ili kupunguza au kuhimili hali hii basi mkurupuko utapatikana...

6. **RADIO PRESENTER:**

sasa tutatumia njia gani ili kupunguza idadi ya mbu? Inaonekana hivi ni vita vigumu kwa sababu mbu wamekuwa wakiishi na binadamu siku zote...

7. **DR. MUNGA:** Kwa mtazamo wangu.. ni lazima kuwe na mikakati yakutosha.. ya kuzuia ueneaji wa mbu na malaria... tuanze na kuwajibika ndani ya majumba yetu.. tupulize dawa za kuua mbu, mazingira yetu yawe sawa sawia, vichaka tuviamirishe, na nyasi ziadimike katika na pembezoni mwa nyumba zetu, tulale chini ya neti zilizotibiwa au hata kuwasha dawa nyakati za usiku ilikuwaua mbu! Haya yakifanywa kila wakati na kwa utaratibu ufaao basi tutaimiliki malaria na maambukizi yatapunguwa..

8. **MASIKA:** **(SUDDENLY REALISES)**

Huyu sharti awe ni yule yule daktari anayemtibu Karembo... najuta kufanya niliyoyafanya...

9. **RADIO PRESENTER:**

Basi hilo bila shaka linawezekana kwa urahisi.. lakini labda msikilizajiwetu anafikiria (**CHANGES VOICE)** "hawa wanazungumza nini? Mimi mwenyewe sina hata hela za kunulia hizo dawa za mipulizo ya mbu au neti"... utawajibu vipi?

10. **DR. MUNGA:** Muda mwingi hizi neti hupeanwa bure katika hospitali za serikali kwa hisani ya wizara ya afya ili kukinga malaria na hata mipulizo pia hufanywa bure na idara ya afya. Nataka kuwakumbusha wasikilizaji kuwa neti hizi hufanya kazi marudufu iwapo zitakuwa zimetibiwa na dawa ya kuua wadudu kama mbu kwa muda wa miaka 3-5 na na hukinga asilimia 80 ya wanakijiji. Na mpulizo wa ndani ya nyumba hudumu iwapo asilimia 80 ya nyumba katika kijiji zinapulizwa kwa muda wa miezi 3-6. Bila shaka italingana pia na kuta au dawa unayotumia. Dawa ya kemikali aina ya DDT ina madhara hasa ikifuliziwa ndani ya nyumba kwa hiyo hatupendekezi sana na pia tuweke dawa zote mbali na watoto.

11. **RADIO PRESENTER:**

Kama ulivyosikia mpenzi msikilizaji... sasa ni wakati wako kutupigia simu iwapo kuna tashwishi au sintofahamu yeyote kuhusu mada ya leo.. na umuulize mtaalamu dkt Munga ambaye

tuko naye hapa kituoni..juma lijalo tutawaletea maafa ya malaria katika eneo letu. Laini zetu za simu ziko wazi au tutumie arafa ya ujumbe mfupi kwa nambari..

12. **MASIKA:** **(REGRETTABLY)**
Natamani kama ningeliweza kuuliza lakini sina simu ya kupiga... lakini nitakuja kukuuliza ana kwa ana kesho nikija kumtembelea binti yangu hospitali...

13. **C-SFX: RADIO BEING TUNED TO ANOTHER STATION**

**NARRATOR:** Masika alijaribu kulaza maungo yake kitandani huku mbu wakimn'gong'a na kumzingira, kisha ghafla wazo likamjia na akalitekeleza mara moja na baadaye akalala fofofo. Asubuhi na mapema siku iliyofuata Mizanja alipata mgeni ambaye alikuwa anamfahamu sana..

**SCENE TWO:MAMA DAVID AT MIZANJA'S SHRINE**

**(MIZANJA CHANTING AND SINGING IN A LOCAL DIALECT)**

14. **MAMA DAVID:** Nakisalimu ewe Mganga wa waganguzi Mizanja! Tabibu wa vizazi vyote!

15. **MIZANJA:** Umeletwa na nini? Shida gani?

16. **MAMA DAVID:** La! Sio mimi, nilikuja kuulizia kwanini wale wageni niliowatuma siku ile hawakutibiwa...kwani nilikosea kuwa na imani na wewe? Hivi sasa

hawesemi tena na mimi!!

17. **MIZANJA:** Hebu nisikilize kwa makini...sisi tunafuata njia za mababu zetu tunapotibu maradhi, lakini pia tunakubali kuwa madaktari pia wana uwezo wa kugangua maradhi haya... kwa hivyo familia ile ilihitaji daktari sio mganga wa kienyeji... mimi ningelitoa mapepo lakini utabibu ungelitoka hospitali.

18. **MAMA DAVID:** **(SHOCKED)**
Kwa hivyo hakuna utata nikipata matibabu mengine ambayo si haya ya kienyeji? Basi nikifikiri kuwa..

19. **MIZANJA:** Mgonjwa huhitaji jambo moja tu.. tiba! Haijalishi ni kutokana na mizizi michungu au dawa zilizo tamu... malengo yetu ni sawa... mgonjwa atibike kutokana na ugonjwa wake! Tunaweza kupishana kwa mambo mengi lakini sote tunakubali kuwa uhai ni dhamana! Na ni lazima ulindwe kwa hali na mali... mimi mwenyewe huwahimiza wagonjwa wa malaria kwenda hospitali baada ya kuwapa mafusho ya kupunguza homa...

20. **MAMA DAVID:** **(SHOCKED)**
Eti nini?..La..hapana,siamini!

**NARRATOR:** Najua msikilizaji, huwezi kuamini lakini hatuwezi kupuuza umuhimu wa waganga wa kienyeji katika vita hivi dhidi ya malaria. Kwani

wengi walioko afrika bado huamini kwamba malaria ikiwa kali mno eti ni pepo hivyo basi huwapeleka wagonjwa wao kwa waganga kama vile mizanja alafu ndio waende hospitali. Bila shaka ni muhimu sana iwapo hata waganga pia watakuwa pamoja kusukuma gurudumu hili la kukinga malaria. Sasa tukiwa katika panga za Mizanja tunajiunga na Masika akiwa hospitali akiwa na bibi yake na watoto wao Zawadi na Karembo...

**SCENE THREE: MASIKA AT HOSPITAL WITH HIS FAMILY**

21. **D-SFX: CUTLERY SOUNDS AS WHEN PEOPLE EAT BREAKFAST**

22. **BETTINA:** Hii ni mara ya kwanza kumuona Karembo akimaliza chakula chake tangu auguwe.. Dkt Munga alisema kuwa alipona kwa haraka alipomtahini leo, na tunamsubiri atueleze kama karembo ataweza kurudi nyumbani leo au ni vipi....

23. **KAREMBO:** Mimi nishapoa,ningelipenda sana kurudi nyumbani... natamani kurudi shule na pia nimewakosa marafiki zangu.. pia mitihani iko karibu.

24. **BETTINA:** Twajua Karembo, lakini ni muhimu kwanza upone.. ulisikia vile Dkt Munga alivyosema, ni lazima umalize dawa zako ndio vimelea vyote vya malaria viangamie... lau sivyo itakurudia...

25. **E-SFX: ZAWADI/BABY MAKES SOME HAPPY NOISES AS MASIKA**

**TRIES TO TALK TO HIM**

26. **MASIKA:** Na Zawadi anaendeleaje? Aliwaweka macho usiku kutwa ama?

27. **BETTINA:** Ah wapi, alilala zii kama gogo,hata mimi pia. Si waona hapa madirisha yamewekwa neti ilikuzuia mbu. Ni muhimu uiregeshe neti yetu Masika.

28. **MASIKA:** Mama watoto,usiwe na wasiwasi.kila kitu tayari.

29. **F-SFX: CURTAINS BEING DRAWN FROM ONE SIDE**

30. **NURSE:** samahani kwa kuwaingilia, Karembo uko na mgeni.. lakini acha kwanza nikutazame joto la mwili na dkt pia anakuja kukuona. Tafadhali hebu weka kipimajoto katika kwapa lako na ukizuie..

31. **MASIKA:** Habari ya asubuhi mkunga,huyo mgeni ni nani?

32. **NURSE:** **(CALLS OUT)**
Tafadhali ingia... sasa karembo hebu nipe hicho kipimajoto..
**(CHECKS IT)**
vyema kabisa... sasa joto limekuwa kawaida... inaonekana homa imekwisha. Haya chukuwa dawa na maji unywe..

33. **G-SFX: TWO GULPS OF WATER.**

34. **KAREMBO:** **(MAKES AN UNPLEASANT SOUND)**
Bwaaaah! Sipendi hizi dawa.

35. **H/TEACHER:** Lakini hio ndio njia pekee yakupata afueni... habari zenu nyote.. mimi ni mwalimu mkuu wa karembo... nilisikia amelazwa kutoka kwa mwanafunzi wetu mmoja... david, nafikiri munamjuwa... pia ilikuwa sadfa kwani nilikuwa nataka kuja kumuuliza dkt Munga aje shuleni ili kutuzungumzia kuhusu malaria. Na amekubali kuja.

36. **BETTINA:** Twashukuru kwa kumtembelea karembo...

37. **KAREMBO:** Ndio twashukuru kwa wema wako.

38. **H/TEACHER:** Sasa naomba kuwaacha ili nisichelewe shuleni.. karembo ninafurahi unaonekana nafuu sasa... pona haraka urudi shuleni.

39. **DR. MUNGA:** (**CHEERFULLY)**
Habari za asubuhi!

40. **H/TEACHER:** Aha, Dkt. Munga, nilikuwa tayari naondoka tafadhali usisahau kuhusu kuja kwa mazungumzo na wanafunzi.

41. **DR. MUNGA:** Sitosahau,kwaheri mwalimu..na huyu mgonjwa wetu anaendeleaje sasa? **(SOUND OF PAGES**

**BEING FLIPPED)** habari zenu? Mgonjwa wetu anasemaje? inaonekana uko tayari kurudi nyumbani sasa, hakikisha umejikinga na mbu wasikuume... na ukisikia ishara ya malaria inakurudia...rudi hopitali haraka tuichunguze! Kuna swali lolote?

42. **MASIKA:** Naam mimi nina swali Daktari.

**MUSIC INTERLUDE**

**OUTRO/NARRATOR**:Basi kabla ya swali hilo kuulizwa na mgonjwa wetu karembo anapopata nafuu tunafikia mwisho wa kipindi chetu cha saba katika mchezo wa kuigiza **"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA"** Je masika anataka kuelezwa nini?na Karembo atapokelewa vipi shuleni? Amejifunza nini katika msimu wa maradhi hayo na atachukua uamuzi gani siku za usoni? Kwa hayo na mengineyo, jiunge nasi katika kipindi kijacho. Unapotaka kusikiliza tena au kutupa maoni yako tafadhali tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe
Hadi wakati mwengine,kwaheri.